



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



HALMASHAURI YA WILAYA MULEBA

Barua zote zitumwe kwa:

Simu: +255 28 2224013

Mkurugenzi Mtendaji (W)

S. L. P 131,

Faksi: +255 28 2224168

Muleba, Kagera

BaruaPepe: ded@muleba.go.tz

Unapojibu tafadhali taja

Kumb. Na. KGR/MLB/HW/A.225/VOL.IV/50

Tarehe: 30/08/2021

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Muleba anapenda kuwatangazia wananchi wote nafasi za kazi ya ajira kwa Watendaji wa Vijiji III nafasi 2

JINA LA KAZI MTENDAJI WA KIJIKI III (NAFASI 2)

A. MAJUKUMU

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- ii. Kusimamia ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji,
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- vi. Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali,
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalam katika Kijiji
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka zote
- ix. Mwenyekiti wa kikao cha wataalamu waliopo katika Kijiji

- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi
- xi. Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za Kijiji na
- xii. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

B. SIFA YA MWOMBAJI

- i. Awe na elimu ya kidato cha IV/VI
- ii. Awe amehitimu masomo ya Astashahada/Cheti katika fani ya Utawala, sheria, Elimu ya jamii, usimamizi wa fedha, Maendeleo ya jamii na Sayansi ya Jamii kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali

C. NGAZI YA MSHAHARA TGS B

D. UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI YA NAFASI ZA KAZI

- i. Barua za maombi ziandikwe kwa mkono
- ii. Barua za maombi ya nafasi za kazi ziandikwe kwa

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

HALMASHAURI YA WILAYA,

S.L.P 131,

MULEBA.

iii. MWOMBAJI AAMBATANISHE


- Curriculum Vitae (CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika
- Nakala za vyeti vya Elimu Sekondari na Chuo
- Hati ya kuzaliwa (Birth Certificate)
- Picha moja ya "PASSPORT SIZE" ya hivi karibuni
- Nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA)

iv. MAMBO YA KUZINGATIA

- Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
- Barua za uthibitisho/matokeo ya mitihani (Testimonials/provisional/statement of result hazitapokelewa.

- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU na NECTA)
- Waombaji waliostafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi
- Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

MWISHO WA KUPOKEA BARUA ZA MAOMBI HAYO NI TAREHE 14/09/2021 SAA 4:00 Asubuhi.


ELIAS M. KAYANDABILA,
MKURUGENZI MTENDAJI (W),

MULEBA

